https://dspace.org/

Siyasa ni tanga si nanga’ mwangwi wa funzo la kisiyasa na azimiyo la abdilatif abdalla kifungoni: Utafiti kiyelelezo wa kutendana katika sauti ya dhiki

Karama, Mohamed; Mwamzandi, Issa; Kitito, Khalid

2020
Jarida la Afrika mashariki la masomo ya Kiswahili
https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144
Karama, M., Mwamzandi, I., & Kitito, K. (2020). ‘Siyasa ni Tanga si Nanga’Mwangwi wa Funzo la Kisiyasa na Azimiyo la Abdilatif Abdalla Kifungoni: Utafiti Kiyelelezo wa Kutendana Katika Sauti ya Dhiki. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 2(1), 28-44.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

East African Journal of Swahili Studies, Volume 2, Issue 1, 2020
Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 2, Issue 1, 2020
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

‘Siyasa ni Tʰanga si Nanga’ Mwangwi wa Funzo la Kisiyasa na Azimiyo la Abḏilaṯif Abḏalla Kifungoni: Uṯafiṯi Kiyelelezo wa Kutendana Katika *Sauti ya Dhiki*[1]

Dkt. Mohamed Karama[1], Prof. Issa Mwamzandi[1] & Khalid Kitito[2]*

[1] Chuwo Kikuu cha Kabianga, SLP 2030 – 20200, Kericho, Kenya.
[2] National Museums of Kenya Heritage Training Institute.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mkarama@kabianga.ac.ke.

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

Tarehe ya Uchapishaji:

27 Apr 2020

Maneno Muhimu:

Siyasa, Abḏilaṯif Abḏalla, Siyasa ni Tʰanga, Sauti ya Dhiki, Uhistoriya.

MUKHṮASARI

Shairi la Kutendana katika *Sauti ya Dhiki* limechanganuliwa, mpaka sasa, kwa maono ya juujuu kwamba ni shairi la kingono. Kuṯokana na hiṯimisho hili, Mulokozi amelipuuza kuwa ni shairi lililokosa ubingwa wa kuenreleza maudhui muhimu yanayotatiza jamii. Makala haya yamebayanisha shairi hili kuwa ni fumbo la kisiyasa. Kwa kutumiya madhumuni ya ulingamanishaji wa fasiri ya matukiyo halisi ya kisiyasa katika Kenya wakaṯi huwo na shairi lenyewe; azimiyo la Abḏilaṯif katika shairi lenyewe na namna lilivofikiwa; na namna azimiyo hilo lilivoathiri msimamo wake wa kisiyasa baaḏa ya kuṯoka kifungoni, tumeweza kuibuwa maswala muhimu kuhusu maisha ya Abḏilaṯif kabla, wakaṯi wa, na baaḏa ya kuṯoka kifungoni. Nadhariya ya Usemezano yenye kuḏulisha maana kuṯokana na usuli, athari, na mwingiliyano wa kauli nyingi katika maṯini na Uhistoriya Mpya yenye kuṯowa fasiri ya matukiyo ya kihistoriya nrizo nadhariya zilizotumika katika uchanganuzi wetu. Kauli mbalimbali zilizojiṯokeza katika mashairi kadhaa ya *Sauti ya Dhiki* na jazanra zilizotumika zimeweza kufumbuwa isṯiyara ya shairi hili la Kutendana. Tumeona wahusika wake (wanawake wawili) wanawakilisha vyama va kisiyasa va wakaṯi huwo: KANU (KADU), KPU, na Mwanamume anawakilisha wananchi wa Kenya. Tukiengezeya, Abḏilaṯif anajisaili huko gerezani na kupelekeya afanye azimiyo la kujiṯowa katika siyasa za kijumuiya sizisothabiṯi na kuwanasihi wasomaji wengine wasiingiye katika mtego

[1] Twamshukuru ghaya Abḏilaṯif Abḏalla, Mungu Atuwekee, kwa kutufunguliya makṯaba yake na kutusaiḏiya kila anḏiko tulilohiṯajiya kwa uwandishi wa makala haya. Piya, twamshukuru Ḏkt. Ahmed Hussein wa Pwani University kwa msaaḏa wake katika kufaulisha makala haya.

aliyouwingiya yeye. Maisha yake ya kisiyasa baaḏa ya kifungo yanaonekana kufuwata funzo na azimiyo hili.

UNUKUZI WA APA

Karama, M., Mwamzandi, I., & Kitito, K. (2020). 'Siyasa ni T^{h}anga si Nanga' Mwangwi wa Funzo la Kisiyasa na Azimiyo la Abḏilaṯif Abḏalla Kifungoni: Uṯafiṯi Kiyelelezo wa Kutendana Katika Sauti ya Dhiki. *East African Journal of Swahili Studies*, *2*(1), 28-44. https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

UNUKUZI WA CHICAGO

Karama, Mohamed, Issa Mwamzandi, and Khalid Kitito. 2020. "'Siyasa ni T^{h}anga si Nanga' Mwangwi wa Funzo la Kisiyasa na Azimiyo la Abḏilaṯif Abḏalla Kifungoni: Uṯafiṯi Kiyelelezo wa Kutendana Katika Sauti ya Dhiki". *East African Journal of Swahili Studies* 2 (1), 28-44. https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144.

UNUKUZI WA HARVARD

Karama, M., Mwamzandi, I. and Kitito, K. (2020) "'Siyasa ni T^{h}anga si Nanga' Mwangwi wa Funzo la Kisiyasa na Azimiyo la Abḏilaṯif Abḏalla Kifungoni: Uṯafiṯi Kiyelelezo wa Kutendana Katika Sauti ya Dhiki", *East African Journal of Swahili Studies*, 2(1), pp. 28-44. doi: 10.37284/eajss.2.1.144.

UNUKUZI WA IEEE

M. Karama, I. Mwamzandi, and K. Kitito, "'Siyasa ni T^{h}anga si Nanga' Mwangwi wa Funzo la Kisiyasa na Azimiyo la Abḏilaṯif Abḏalla Kifungoni: Uṯafiṯi Kiyelelezo wa Kutendana Katika Sauti ya Dhiki", *EAJSS*, vol. 2, no. 1, pp. 28-44, Apr. 2020.

UNUKUZI WA MLA

Karama, Mohamed, Issa Mwamzandi, and Khalid Kitito. "'Siyasa ni T^{h}anga si Nanga' Mwangwi wa Funzo la Kisiyasa na Azimiyo la Abḏilaṯif Abḏalla Kifungoni: Uṯafiṯi Kiyelelezo wa Kutendana Katika Sauti ya Dhiki". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 2, no. 1, Apr. 2020, pp. 28-44, doi:10.37284/eajss.2.1.144.

UTANGULIZI

Wakaṯi wa mazishi ya nruguye mkubwa Usṯadh Ahmaḏ Nassir mjini Mambasa Januari 2019, tulipata bahaṯi ya kukutana na Abḏilaṯif Abḏalla na katika maongezi yetu naye kuhusu Kiswahili na mengineo alitwambiya kuwa babu yake marehemu Mzee Hyḏer Kinḏy nriye aliyemwambiya kwamba siyasa ni t^{h}anga si nanga alipoṯoka kifungoni 1972. Msemo huu ni kama naswaha ya babu yake kwake lakini piya ni uṯabiri wa msimamo wake kuhusu siyasa ya kijumuiya. Msimamo wa Abḏilaṯif katika siyasa ni wa kiuwanaharakaṯi ṯangu miyaka ya siṯini ya karne iliyopita. Kwa kutumiya shairi Kutendana linalopatikana katika *Sauti ya Dhiki* (SyD), ḏiwani aliyoitunga akiwa kifungoni, makala haya yanaonesha kwamba msimamo wake wa siyasa ya kijumuiya uligeuka alipoṯoka kifungoni. Mabaḏiliko haya yaliṯokana na uṯanabahisho aliyoupata akiwa kifungoni baaḏa ya kujisaili na kujaḏiliyana na nafsi yake kama alivowasilisha katika shairi hili na mengineo katika ḏiwani hiyo.

Kazi kadhaa zimeanḏikwa kuhusu harakaṯi za kisiyasa za Abḏilaṯif, kwa mfano, Beck & Kresse (2016), kuhusu mashairi yake tukitaja wachache: Maitaria & Wafula (2018), Vierke (2017), Hamad (2017), Khamis (2016), Karanja (2014), Mwamzandi (1996), Topan (1994), Chacha (1992), Senkoro (1988), Gibbe (1978), Mulokozi (1975), Ohly (1974). Woṯ^{h}e hawa wameyashughulikiya mawazo yanayojiṯokeza katika mashairi yake na piya fani mbalimbali alizotumiya wakaṯi wa uwasilishaji wa mashairi yenyewe. Kati ya hawa kuna waliyoshughulikiya uṯamthiliya unavojiṯokeza katika mashairi ya Abḏilaṯif kwa mfano, Topan, Senkoro, Chacha, Ohly, Mwamzandi. Na kati ya hawa waliyoshughulikiya uṯamthiliya kuna waliyoshughulikiya kwa njiya moja au nyengine shairi la Kutendana, kwa mfano, Mwamzandi, Chacha, Senkoro, na Ohly.

Mwamzandi alijimakinisha katika kuonesha mbinu za kiṯamthiliya zinazojiṯokeza katika shairi hili. Senkoro na Chacha walijishughulisha zaiḏi na maudhui yanayopatikana na Ohly aliziḏi kiḏogo kwa kuangaliya uṯamthiliya na 'uṯaalamu' wa Abḏilaṯif uliyomo. Woṯ^{h}e hawa walichambuwa shairi hili katika maudhui ya juujuu yanayojiṯokeza wazi: ni ngonjera ya mwanamume mwenye uchu wa kuṯekeleza haja yake ya maṯamaniyo ya nafsi na kukataliwa na mwanamke. Kwa minṯarafu ya

East African Journal of Swahili Studies, Volume 2, Issue 1, 2020
Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

uchanganuzi wa aina hii, Mulokozi akinukuliwa katika Chacha (1992) anasema kwamba Kutendana ni shairi dhaifu kwa kukosa usanifu na maudhui yenye lengo la kuusaiḏia ummah. Makala haya yaṯaipinruwa kauli ya Mulokozi tuliyoitaja kwa kuonesha kwamba ngonjera hii ni isṯiyara na ina maana ya zaiḏi kuhusu Abḏilaṯif kisiyasa.

UHISTORIYA NA SYD

Fasiri yetu ya shairi la Kutendana imebayanika kwa kuegemeya maelezo ya nadhariya ya Usemezano inayoiṯifakiwa ni Mikhail Bakhṯin na Uhistoriya Mpya inayoiṯifakiwa na Stephen Greenblatt. Kulingana na Bakhṯin (1981) neno likiangaliwa kikamusi basi hujulisha maana ya juujuu na yaweza kuwa hiyo siyo maana haswa iliyokusuḏiwa katika mtongoo huwo. Kulingana na yeye, ukiṯaka maana haswa ya neno lazima uliyangaliye kwa mawanḏa mapana huku ukitiliya maanani usuli, historiya, uṯamaḏuni, mukṯadha wa matumizi, viimbo va sauṯi, na ikiwezekana niya ya msemaji wake. Vigezo hivi lazima vitiliwe maanani wakaṯi wa kuṯafuṯa maana ya neno kwa sababu neno lina athari za kule liṯokako na ni mwangwi wa neno lengine. Mwangwi huu waweza kuwa wa neno lililosemwa huko nyuma na laweza kuathiri maneno yaṯakayokuja baaḏaye kwa kuwa maneno yana sifa za kijamaa, yaani, huathiriyana na kuchangiyana kiubavuni, kimbele na kinyuma. Kuṯokana na maelezo haya basi kipashiyo kinachochunguzwa hapa si neno bali ni kauli. Ni kauli kwa sababu kuna vigezo vingi vinavotiliwa maanani ili kupata maana. Hali kadhalika, fikra za wanauhistoriya mpya ni kwamba matukiyo ya kihistoriya katika fasihi hupawa fasiri ili maana yake ijiṯokeze katika mfanyiko mzima wa matukiyo hayo ya kihistoriya katika jamii (Tyson, 2006; Habib, 2005). Kwa minṯarafu hiyo, kauli ainaṯi alizozitumiya Abḏilaṯif katika mashairi yake yoṯ^{h}e katika ḏiwani hii, kama alivoainisha Walibora (2009), pamoja na namna mawazo yanavojumuishana na kuchangizana nriyo iliyochangiya kuvumbuwa maana ya nrani ya shairi hili.

MIPAKA MIPYA YA SYD

Kufikiliya lengo la makala haya tumetumiya madhumuni mat^{h}atu: Ulingamanishaji wa matukiyo halisi ya kisiyasa katika Kenya wakaṯi huwo na shairi lenyewe; azimiyo la Abḏilaṯif katika shairi na namna lilivokuja; na namna azimiyo hilo lilivoathiri msimamo wake wa kisiyasa baaḏa ya kutoka kifungoni. Madhumuni haya yalituwezesha kulielewa kwa mapana shairi la Kutendana na kuyaelewa maisha ya kisiyasa ya Abḏilaṯif kifungoni na baaḏa yake. Hali kadhalika, katika uchanganuzi wetu hatukufuwata ṯarehe zilizoanḏikwa kila baaḏa ya shairi kwa sababu t^{h}atu. Mosi, ni kwamba ṯarehe zingeleta mipaka ya kiwakaṯi baina ya mashairi na hivo kuleta mipaka na ṯafauṯi katika maisha mazima ya Abḏilaṯif kifungoni. Pili, ni kwamba ṯarehe zenyewe zaweza kuwa (si kwa kusuḏi la kupotosha) zimepachikwa kwa sababu zina ṯashwishi usahihi wake. Mfano, katika ḏibaji ya SyD, Abḏilaṯif anasema kwamba alilitunga shairi "Moyo Iwa na Subira" ṯarehe 20/10/1971 lakini ukienra kiṯabuni shairi hili hili imeanḏikwa lilitungwa ṯarehe 20/3/1971.

T^{h}atu, ni kwamba mashairi yenye mtinro wa uchanganuzi na uṯathmini, kama hili Kutendana, yameonekana kuwa marefu zaiḏi na yenye toni tulivu kuliko mashairi aliyotunga mwanzo mwanzo yaliyojaa hasira na ni mafupi. Kwa hivo, yaweza kuwa mashairi ya kiuchanganuzi hayakutungwa katika ṯarehe zilizoambatishwa nayo. Kwa sababu hizi, sisi tuliamuwa kutumiya mawako ya mashairi yenyewe kimpangiliyo kiṯabuni na kuyaita kwa majina yaliyopawa na mtunzi na kuwa yako mwanzo, kati au mwisho wa kiṯabu. Hili lilitusaiḏiya kuonrowa mipaka ya kiwakaṯi na kufuwata mahali yalipo na kuwacha mawazo yaingiliyane bila mipaka kama inavojulisha nadhariya ya Usemezano. Aidhan, katika makala haya tumetumiya maana finyu ya fasihi ya ufungwa, kama ilivorejelewa na SaiD & Taib (2019), ili tuangaziye namna gereza (mahali haswa siyo fikira au dhana) lilivoweza kumbaḏilisha Abḏilaṯif baaḏa ya ṯaḏaburi ya maisha yake na ya jamii yake. Katika makala haya neno siyasa ya kijumuiya inamaanisha siyasa ya wat^{h}u waliyoko katika jamii yake na ya Kenya kwa ujumla. Piya shairi la Kutendana liṯarejelewa sawiya kama ṯamthiliya ya (mchezo wa) Kutendana na maana ni ile ile moja.

Sisi tulijiuliza maswali kadhaa kuhusu shairi hili na changanuzi hizi zilizoutanguliya uṯafiṯi wetu: Je, fasiri ya shairi hili ni hii pekee? Je, mbona shairi kama hili la kimapenzi (kiudhahiri) lipatikane katika ḏiwani yenye ghamidha ṯangu shairi la

mwanzo Nshishiyelo ni lilo! haḏi la mwisho Nsharudi? Je, shairi hili laweza kuwekwa wapi katika maisha mazima ya Abḏilaṯif kifungoni? Je, kuna sababu zozoṯʰe zinazojiṯokeza ḏiwanini zilizochangiya haḏi Abḏilaṯif akalitunga? Kwa nini Abḏilaṯif amaliziye shairi/ ṯamthiliya kwa maneno /Jaribu kuyaepuka, haya uliyosoma nyuma/? Je, mbona kuna msimamo huu katika shairi hili na haswa katika shairi la mwisho? Maswali haya yalitusaiḏiya kulichanguwa upya shairi hili na kubaini kwamba kuna fasiri ya ziyaḏa siyo ile iliyojitokeza waziwazi. Chembelecho Walibora (2016) ukiyaangaliya mashairi ya Abḏilaṯif kijuujuu uṯayaona ni mepesi lakini yaṯaka makini kuchunguza maana za nrani zilizojifiṯa.

UFUPISHO WA KUTENDANA

Ploti kuu inayojiṯokeza katika shairi hili ni mwanamke anamkataliya kumṯimiziya haja ya kingono mwanamume wake kwa sababu amechoshwa na ṯabiya zake mbaya. Mwanamke anamfunuliya Mwanamume uwovu aliyoufanya kwa kumgeuka mtʰu (Mwanamke) ambaye amefanya kila kitu kuliweka penzi lake kwa mwanamume huyo. Amempa kila chake mpaka akiba yake yoṯʰe na zaiḏi akakopa kwa watʰu na kuweka rahani vombo vake va dhahabu na vengine va thamani alivokuwa navo ili amkimu huyo Mwanamume. Mwanamke anaiyona hiyo ni hiyana aliyofanyiwa na Mwanamume wake kwani kila akipata mshahara wake hakumsaiḏiya huyo Mwanamke. Bali zaiḏi, huyo Mwanamume alikwenra kwa mwanamke mwengine kwa jina Mishi kufanya mapenzi naye na mshahara wake aliupeleka kwa huyo mwanamke mwengine. Haṯa hivo, huko kwa Mishi huyo Mwanamume alifukuzwa baaḏa ya kuonekana hana kitu cha kuṯowa. Mwanamume anabaki ameḏangana majiyani hajijuwi hajitambuwi baaḏa ya kufukuzwa koṯe kuwili.

Kifani shairi hili linaṯafauṯiyana na mashairi mengine (isipokuwa Mnazi) katika SyD kwa kuwa limeunrwa kiṯamthiliya au kingonjera. Ni masemezano baina ya "wapenzi" wawili – Mwanamke na Mwanamume. Ni mapenzi ya kukoḏisha kwa sababu si wananrowa; hakuna mahali shairini wanaitwa mume na mke wa mtʰu. Ṯamthiliya yenyewe inaanza mbele wakaṯi Mwanamke anamkataa Mwanamume halafu baaḏaye, kwa mbinu rejeshi, tunaoneshwa namna mchezo ulivoanza. Nrani ya mchezo wenyewe kuna maelezo ya msimulizi ambaye anaingiya mara kwa mara kutueleza zaiḏi kuhusu matukiyo mchezoni. Katika ṯamaṯi ya ngonjera hii, msimulizi anatupa uchanganuzi wa kuyapima makosa yaliyoṯokeya baina ya wahusika hawa watʰatu: Mwanamke, Mwanamume, na Mishi. Piya kuna matumizi ya maelezo katika akili za wahusika na lugha ya mchezo ni nyepesi yenye toni ya ghadhabu.

USULI WA KAULI ZA SYD

Msomaji wa kazi ya Salim (1975) aṯafunukiwa na ṯaharuki iliyokuwako nchini Kenya (haswa katika Mkowa wa Pwani) muḏa kiḏogo kabla ya kujinyakuliya uhuru wake kuṯoka kwa wakoloni Waingereza. Waswahili na Waarabu walikuwa na wasiwasi kuhusu Kenya iṯakuwaje baaḏa ya uhuru na hivo kuziwacha jamii hizi mbili katika hali ya kuṯojuwa kuchukuwa haṯuwa ipi katika kujiweka makini katika maswala ya kisiyasa. Vile vile, ubaguzi na uwonevu wa kikabila ulokuwako wakaṯi wa ukoloni, kama anavoeleza Kindy (1971), uliwawaṯa Waswahili katika njiya panra ya kuṯojuwa wajitambulishe ni Waafrika, ambapo hawafaiḏiki kimaslahi yao, au, wajiite Waarabu, ambawo walikuwa na saṯwa afadhali kwa wakoloni japokuwa waarabu wenyewe walikuwa hawawaṯaki hawo Waswahili. Kinḏy ambaye ni babu yake Abḏilaṯif ni mmoja kati ya Waswahili waliyojiṯowa waziwazi kwamba yeye ni Mswahili na ni mwafrika mwanaṯʰi wa Mambasa. Piya alikuwa mwanaharakaṯi shupavu dhiḏi ya ubaguzi wa aina yoyoṯʰe na alikuwa mwanasiyasa. Nruguye Abḏilaṯif, Sheikh Abḏillahi Nassir, alikuwa shekhe na mwanasiyasa na kati ya waanzilizi wa chama cha KANU, chama ṯawala baaḏa ya uhuru. Hivo, Abḏilaṯif alilelewa na kukuliya katika familiya ya wanasiyasa, nripo sana, naye akainukiya kuwa mwanaharakaṯi wa kisiyasa.

Maswala haya ya kisiyasa hayakukomeya hapa, kwani Kenya ilipojinyakuliya uhuru wake wa kisiyasa baaḏa muḏa kiḏogo ṯu, 1964, mambo yalikuwa yashachacha na makunri yashaanza kujiṯokeza kuipinga serikali changa ya Jomo Kenyatta. Kulikuwa na KANU cha Jomo Kenyatta, KADU cha Ronald Ngala, na kisha KPU (kilichounrwa 1966) kilichoongozwa na Oginga Odinga. Makunri haya yalizozana kisiyasa na kila

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

mmoja akimwona mwenziwe hafanyi kazi. Odinga katika ṯawasifu yake *Not Yet Uhuru* (1968) anayaeleza matukiyo ya kisiyasa kabla na punre ṯu baaḏa ya uhuru kwa uketʰo na kuonesha namna wenzake wachache, serikalini na nje ya serikali, walivowacha kuwatumikiya wananchi wanyonge na kufuwata njiya ya kujiṯajirisha wao kwa haraka na kubaḏili mipango yoṯʰe mizuri walokuwa wameyapanga kuwanufaisha wananchi wanyonge waliyo wengi. Abḏilaṯif alijiunga na chama hichi cha KPU kwa sababu ya kukiyona chapiganiya haki halisi za mwananchi wa ṯabaka la chini kiuchumi. Alikuwa mwanachama kijana mshupavu na akaonekana kuwa mfuwasi barabara wa chama hicho. Alipawa wadhifa wa kuanḏika makala ya kila mwezi kuhusu siyasa ya chama na harakaṯi zake katika Mkowa wa Pwani lakini aliyafanya yoṯʰe kichinichini huku akiwa karani wa Mansipaa ya Mambasa.

Alianza kuchapisha kijumbe kiitwacho *Kenya Twendapi?* kilichoelezeya madhila yanayowapata wakenya kuṯokana na uṯawala mbaya wa chama cha KANU. Alipata usaiḏizi wa kuchapisha makala haya kuṯoka kwa wanachama wengine walomsaiḏiya kwa mashini ya kuchapisha na wengine walisaiḏiya kuyasambaza makala hayo katika pembe zoṯʰe za mkowa (Kresse, 2016). Aliyafanya kwa siri sana na mara ya mwisho wasimamizi wa mkowa walikuja kumuonya mara kadhaa ajiyepushe na kazi hiyo lakini alikataa kusimamisha shughuli hizo. Mwishowe, nruguye mkubwa Sheikh Abḏillahi Nassir alimṯahadharisha na kumuonya aṯakuja kushikwa. Abḏilaṯif alimwambiya nruguye kwamba aṯaenreleya na msimamo huwo na hakimbii bali zaiḏi wanaloweza kumfanya hawo wanaomwanḏama ima waṯamfunga au waṯamuuwa (*Kenya Twendapi?* katika youtube.com). Hakuṯoroka kwenra kokoṯʰe bali walikuja maafisa wa upelelezi baaḏa ya kupawa fununu na mwenḏani wake (nriye aliyemsaliṯi) kuwa nriye mchapishaji wa makala hayo. Wakaisaka nyumba yake na wakapata nakala moja ṯu ya chapisho hilo la *Kenya Twendapi?* (Kresse, khj.). Katika chapisho hili la sabaa la 1968 nrimo Abḏilaṯif alipowahamasisha wananchi wasimame kuchukuwa haki yao haṯa kama ni kwa kutumuiya nguvu (kwa silaha). Kauli hii nriyo aliyoshiṯakiwa nayo kwamba alihaṯarisha amani na usalama wa nchi.

Maisha Humo Gerezani

Katika kazi ya Adam Shafi ya *Haini* (2003) anayaeleza maisha ya kifungoni kwa kina na anawasilisha ṯaswira ya maisha madhalilifu anayokumbana nayo mfungwa katika jela za huku kwetu Afrika. Katika mateso makubwa anayopawa mfungwa yoyoṯʰe ni kufungwa peke yake – hajuwi ni mchana ni usiku, wala hasikii sauṯi ya kitu chochoṯʰe ila ni kuzungukwa na kuta hizo nne, bariḏi shaḏiḏi na maṯambara kuwa vifuniko va mwili wake, hapana kitanra ila sakafu bariḏi. Haya nriyo mapokezi aloyapata Abḏilaṯif alipowekwa kifungoni anapoyaeleza maisha haya katika shairi lake Nshishiyelo ni Lilo.

Kulingana na maelezo aloyaṯowa katika *Africa Events* (1985), Abḏilaṯif anatwambiya kitu cha kwanza alichofanywa alipoingiya jela ni kuvuliwa utʰu wake na uwako wake na kupawa namba (KAM/285/69/LS) kuwa nriyo kitambulisho chake mule gerezani. Ilibiḏi aihifadhi nambari hiyo mara moja na ageuzwe "mtʰumwa" wa kuitika kijeshi kila anaposemezwa. Adhabu za kila aina zilianza wakaṯi huwo huwo. Alipawa kazi ngumu kama kuvunja majabali kwa nyunro mpaka aliwahi kuvunjika mkono wake.

Katika siku za mwanzo mwanzo alikataliwa kuṯangamana na nje yaani kuliyona juwa ila kwa wakaṯi maalumu. Piya, hakuruhusiwa kuzungumza na mtʰu yoyoṯʰe wala kusoma kitu chochoṯʰe. Adhabu kubwa aloiyona yeye ni kuponrwa kisaikolojiya ili ivunje dhamiri yake. Alililamikiya hili kwa wasimamizi wa gereza nao walimkataliya haṯa baaḏaye sana walimpa nakala ya Kiarabu ya *Kuruani*, kiṯabu ki ṯakaṯifu cha Waislamu, wakidhani haṯoelewa kitu nrani yake (Wanjiru, 2010). Anavosimuliya yeye kwamba hii nriyo iliyokuwa zawaḏi kubwa walompa wasimamizi bila ya kujuwa kwamba amepata rafiki wa kuzungumza naye humo jela. Piya, kuṯokana na usuhuba aloufanya na maaskari wa pale gerezani waliweza kumleteya penseli na ikawa piya ni faraja kubwa ya kuweza sasa kuanḏika chochoṯʰe kinachomjiya akilini mwake. Karaṯasi za chooni nrizo zilizokuwa nyaraka zake za kujipumbaza kuanḏika alichokifikiriya siku hizo, nriyo usuli wa utunzi wa mashairi haya ambayo baaḏaye yalikusanywa katika ḏiwani ya SyD. Aliwahi piya kuwa na shajara lake la kimsimbo alilofahamu yeye ṯu

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

alichoanḏika humo kwa jina *Ni Haki Yangu* (Wanjiru, khj.) kuyakumbukiza matukiyo anayokumbana nayo mule kifungoni. Kwa bahaṯi nzuri si nyaraka za hayo mashairi wala si hilo shajara alilopoṯeza wakaṯi wa kuhamishwa kwake kwenra Shimo la Ṯʰewa ziligunruliwa. Abḏilaṯif anatwambiya kuwa mashairi yake aloyaanḏika kifungoni (yoṯʰe isipokuwa Nsharudi aliloanḏika baaḏa ya kuṯoka jela) nriyo yalomliwaza kila alipojiyona aṯaka vunjikwa ni moyo.

Kuṯokana na maelezo haya tunaupata mukṯadha kamili wa Abḏilaṯif alivoingiya katika siyasa kuṯokana na sababu za kihistoriya zilizokuwako wakaṯi huwo. Ṯaharuki ya kisiyasa, ubaguzi wa kikabila, na kuṯowajibika kwa serikali kuhusu wananchi wake. Piya tumeona kuwa Abḏilaṯif alijiṯoleya kwenreleza shughuli za chama chake KPU kwa ukamilifu na kwa moyo mmoja. Alijiṯoleya kwa mali (kupata mashini, watʰu wa kuchapisha na kusambaza mkowani) na hali – kutumiya wakaṯi wake kuanḏika na kueleza dhuluma za chama cha KANU na serikali na mikakati ya chama chake KPU. Zaiḏi, alikuwa ṯayari kufungwa au kuuliwa, ikiwa iṯafikiya haḏi hiyo, lakini hawachi kukitumikiya chama na ummah. Baaḏa ya yoṯʰe hayo, Abḏilaṯif alikuja kukamatwa, kufunguliwa mashiṯaka, na kuhukumiwa kifungo kwa uchochezi. Chama chake KPU kilipigwa marufuku na Odinga alifungwa kifungo cha nje. Chama cha KANU kikaenreleya kuṯawala kama serikali ya chama kimoja na wanachama wake wachache wakiparamiya mali ya ummah bila kujali. Wananchi alowapiganiya haki yao wakawachwa hohehahe hawana mwangalizi wala mtetezi wa masilahi yao. Kuṯokana na mukṯadha wa ṯaswira hii na mandhari haya tuliyoeleza kuhusu siyasa ya Kenya wakaṯi huwo, nrivo tulivolifafanuwa shairi la Kutendana.

DHANA YA ISṮIYARA

Isṯiyara ni usukaji wa kazi za kifasihi kimafumbo zenye kuficha maana halisi ya mtungaji wa kazi hiyo mpaka msomaji azame zaiḏi katika kazi yenyewe nripo apate kufunukiwa na fasiri mojawapo ya kazi hiyo. Kwa minṯarafu hii ya fumbo, kama yalivo mashairi mengine ya SyD, nriyo shairi la Kutendana yaṯaka liyangaliwe. Topan (2006) anasema ni ṯaabu kupata maana halisi ya fumbo kwa sababu mtungaji hatufunulii yoṯʰe kwa uwazi na mengine inabiḏi tujichotee kuṯokana na habari zijulikanazo kumuhusu mtunzi wa kazi hiyo. Kwa hivo, kwa upanre wetu tumetumiya kauli za wahusika na tukashikanisha na matukiyo halisi ya kisiyasa za wakaṯi huwo nripo tulipoweza kubaini fasiri zaiḏi za shairi hili.

Isṯiyara ya Kutendana

Kama tulivoeleza hapo awali kwamba Kutendana ni fumbo basi fumbo hili limeweza kufumbatwa kwa sababu ya matumizi ya jazanra pevu zilizoficha maana batini ya kauli za mtunzi. Abḏilaṯif katika shairi lake "Mamba" anaṯowa biri ya mtʰu yoyoṯʰe asome mashairi yake na halafu afumbuwe lililokusuḏiwa. Anatwambiya:

1. *Nami nambe, niwe kama waambao*
   Niupambe, upendeze wasomao
   Niufumbe, wafumbuwe wawezao.

Ubeṯi huu unatwambiya Abḏilaṯif anaṯaka kusema maneno yake lakini kwa mafumbo na waṯakaoweza kufumbuwa basi wajaribu. Kwa mnasaba huu nriyo tulifikiriya kuliangaliya shairi la Kutendana kuwa ni fumbo kwa kuwako kwake katika mashairi yaliyotungwa kifungoni ṯena ya siri kubwa. Ni ya siri kwa sababu mfungwa gerezani alikuwa hakubaliwi kusoma chochoṯʰe kisichojulikana na wasimamizi seuze kuanḏika chochoṯʰe.

Isṯiyara ya mapotʰe ya kisiyasa

Katika Kutendana kuna wahusika watʰatu: Mwanamke, Bi Mishi na Mwanamume. Ufumbuzi wetu wa shairi hili ni kwamba Mwanamke anamwakilisha Abḏilaṯif mwenyewe, Bi Mishi ni kiyelelezo cha waporaji wa mali ya umma na kwa kaḏri fulani chama cha KANU, na Mwanamume ni kiyelelezo cha wananchi madhaifu wa Kenya. Tukiangaziya matukiyo ya kisiyasa tuṯaona kuwa katika siyasa ya Kenya wakaṯi huwo haḏi sasa kuna vyama vingi va kisiyasa. Wakaṯi huwo kulikuwa na KANU, KADU, na KPU ambacho nricho chama changa kati ya hivi voṯʰe. Walakini chama cha KADU kilimizwa na chama cha KANU wakaṯi wabunge wake walipoamuwa kukiṯupiliya mbali chama chao na kukubali kuungana na chama cha KANU. KPU kilijiṯokeza 1966 baaḏa ya Oginga Odinga kuwona kuṯowajibika kwa watumishi wa serikali kwa wananchi wao na kuwekwa kanro

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

mipango yoṯʰe iliyokuwa imepangwa kukuza hali ya mwananchi wa ṯabaka la chini.

Kauli na matenro ya Mwanamke katika Kutendana yanaashiriya zaiḏi kuwa ni chama cha KPU kinachorejelewa hapa. Tenro la kujiṯoleya kwake kuhakikisha kwamba Mwanamume anasṯarehe katika maisha yake na kujikusuru yeye ili Mwanamume apate nrivo ilivokuwa kwa wanachama wa KPU – walijiweka nyuma ya wananchi na kuwatanguliza wananchi katika mipango ya maenreleyo. Kauli inayothubuṯisha kwamba ni KPU ni ile kauli ya Mwanamke inayoruḏiwa kuṯoka ubeṯi wa 34 haḏi 55 inayosema, "ṯamaa innishika". Kauli hii ilisemwa na Mwanamke wakaṯi alipomfunuliya Mwanamume wema woṯʰe aliyomfanyiya ili yeye asṯarehe asipate ṯaabu haṯa siku moja. Usemi wa "ṯamaa innishika" ni jawabu ya usemi mwengine kiunrani ya kauli ya "siṯosheki", yaani "mimi sijaridhika". Tukiileta kwa wingi kauli hii "hatuṯosheki" na tukiwarejeleya kwengine tukiuliza, "kina nani hawo?" Iṯajibiwa, "wasiyoṯosheka". Kresse (2016) anasema kauli hii ya "wasiyoṯosheka" nriyo iliyokuwa saini ya makala yoṯʰe waliyokuwa wakiyaanḏika akina Abḏilaṯif ṯena kwa herufi kubwa WASIOṮOSHEKA. Kwa hivo, twaweza kukubali kuwa ni ya Abḏilaṯif kwa ujumla na yaweza kuwa ni ya chama cha KPU kwa uchache. Haṯa hivo, uchanganuzi wetu umekuja kuwona kwamba chama cha KPU hakikuwaambiya wanachama wake wala wananchi waachane na misimamo yao au kuruḏi nyuma katika mapambano na uṯawala wa kunyonya na kunyanyasa wananchi. Kimaoni yetu, kauli hizi /Nyege ni kunyegezana, kwangu huba zinkwisha/ na /Kitʰu n'nachokuṯaka, shairi wishapo soma. Jaribu kuyaepuka, haya ulosoma nyuma/ zinazotumika katika Kutendana ni kauli za Abḏilaṯif binafsi zenye kuashiriya kubaḏili msimamo wake kuhusu siyasa ya kijumuiya. Na matenro yake ya kujiṯowa kwenye uwanḏa wa siyasa kwa muḏa baaḏa ya kuṯoka kifungoni, kama tuṯakavoonesha katika sehemu ijayo, nriyo ushahiḏi unaoshaḏiḏiya maoni yetu kwamba Mwanamke katika Kutendana ni Abḏilaṯif na wala si KPU.

Isṯiyara ya uwanachama wa kisiyasa

Ploti ya Mwanamume kuja kuṯaka kuṯimiziwa na kujiṯosheleza yeye haja yake kingono nriyo ploṯi iliyowashughulisha waṯafiṯi waliyokuja kabla ya uṯafiṯi wetu Wotʰe wameliyangaliya shairi hili na mahiṯimisho yao yakakatikiwa kwamba ni shairi dhaifu kama Mulokozi, na wengine wakalichukuliya kuwa ni shairi la ukombozi wa wanawake, kwa mfano, Chacha (1992). Kipaumbele ilichopawa ploti hii ya ngono nriyo iliyosababisha matukiyo yoṯʰe kuṯokeya katika mchezo huu haṯa Mwamzandi (1996) alilitaja wazo hili. Anakuja Mwanamume kwa Mwanamke wake kujiṯosheleza maṯamaniyo ya nafsi yake na Mwanamke anaamuwa kumkataliya siku hiyo kwa sababu Mwanamke hajaona umuhimu wa wao kuwa pamoja katika penzi hili. Mwanamume analeta maneno na Mwanamke anamfunguliya shajara ya namna alivomsṯahmiliya Mwanamume siku zoṯʰe kwa kumlisha, kumvisha, na kumuweka pahala pasṯahikifu lakini Mwanamume anamchezeya shere Mwanamke huyu kwa kwenra kwa Mwanamke mwengine aitwaye Mishi. Mwanamke anakataa dhuluma hii ya kusahau fadhila na hisani na kumwambiya kuwa sasa ana Mwanamume mwengine anayejiṯayarisha kwonana naye.

Abḏilaṯif amekuliya katika malezi ambayo babu yake mzee Ahmad Muhammad Maṯano na nruguye Abḏillahi Nassir walikuwa ni mashekhe wa Kiislamu katika jamii ya Mji wa Kale, Mambasa. Haṯa Mazrui (2017) amesema kwamba Abḏilaṯif ameweza kuchanganya Uislamu katika mashairi yake yakawa yameumana kama kitu kimoja. Walakini, katika SyD kuna mashairi mawili ambayo ni ya "kiasharaṯi" (sivo amaanishavo Shariff (1988) kwa kuwa halikuanza na maombi kwanza) yenye maudhui ya watʰu ajinabi kuingiliyana kingono jambo ambalo tuṯaṯarajiya kwa kijana aliyeleleka katika ushekhe hawezi kuzungumziya maswala ya kujamiiyana hadharani. Shairi la Usiniuwe! lahusu msichana aliyekwenra kupata mimba kabla hajaolewa na anapoṯaka kuiyavya mimba hiyo kiumbe kilichomo nrani ya tumbo lake chamsihi asikiuwe. Kutendana hali kadhalika, wahusika Mwanamume na Mwanamke piya hawajaowana kishariya (ubeṯi wa 158 /Alifanya sawasawa, Dume kuliangaliya. Na hali huyo hakuwa, mwenzi wake wa shariya?/) bali wamewekana kinyumba (ubeṯi 21 /Siku zote twalokuwa, pamoja tukiwekana/) kama mahawara. Mbali na hayo, shairi lenyewe lina lugha inayofanana na lugha ya maskani – mabaraza wanayokaa vijana mitaani kuzungumza maudhui

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

ainaṯi yakiwamo ya mpira, habari za magazetini, uḏaku wa mitaani, na piya haḏithi za mt^{h}u kukataliwa na Mwanamke. Nilipomuuliza Abḏilaṯif kwa Whatsapp (Oktoba 21, 2019) kama alikuwa kijana wa kishekhe (kwenra msikitini na kuruḏi nyumbani) au alikuwa akikaa maskani na vijana wenzake akanambiya alikuwa na maskani yao Kuze wakikaa na kupiga soga au stori kama wanavoziita wenyewe vijana. Kwa hivo, si ajabu kwamba Abḏilaṯif ametumiya ploti hii ya mapenzi ya mahawara katika Kutendana na msichana kushika mimba kabla hajaolewa katika Usiniuwe kwa sababu nriyo masimulizi "motomoto" wanayoyapenḏeleya wanamabaraza ya vijana.

Tukiileta isṯiyara hii katika matukiyo halisi ya siyasa ya wakaṯi huwo tuṯaona kwamba majumuiko katika maswala ya kisiyasa si ya nrowa za kufa kuzikana, ni maswala ya masilahi kila mmoja kupata yake. Kwa ajili hii, mt^{h}u kuwamo nrani ya chama kimoja leo na kesho yuko chama chengine ni kawaiḏa kisiyasa. Haṯa mapenzi yao ni mapenzi ya kijuujuu yasiyokuwa na mashiko kwa sababu ya masilahi. Isṯiyara hii ya mapenzi ya kijuujuu nriyo ilomfanya Abḏilaṯif kukataa kushirikiyana na wananchi wasiyokuwa na msimamo thabiṯi. Fungamano lake na wananchi ni kuhusu siyasa ya kupiganiya masilahi yao pamoja lakini ikiwa wananchi waṯakwenra kwa mwengine kwa kuḏanganyika basi hawana haja ya kuwako pamoja (Abḏilaṯif na wananchi wa chini). Kwa hivo, jazanra hii ya ngono ni mwafaka kufananisha maingiliyano ya kisiyasa baina ya wanachama na mapenzi ya kihawara ni kiwakilishi mwafaka cha mapenzi ya kuḏanganyana baina ya wanasiyasa na wananchi.

Isṯiyara ya hiyana ya wananchi

Kama tulivoeleza katika sehemu iliyopita kwamba ploti ya ngono na kukataliwa mwanzo wake iliyanza na Mwanamke kujiṯoleya vilivo katika penzi hili. Mwanamke alijiṯoleya kikamilifu kwa lake na chake akampa Mwanamume ili wawe pamoja maishani. Aliuza kila kitu na akiba yake na mwisho akaweka rahani na zaiḏi akaanza kukopa ili apate cha kumfurahisha Mwanamume. Mwanamke anasema hivi:

34. *Nalihikajilifisha, kwamba nipate kuweka*
Hifunguwa langu kasha, kila likihitajika
Nikawa nikikulisha, pamoja na kukuvika
Vipi wanambiya kisha, tamaa innishika?

Haṯa alipokuwa akiyambiwa usifanye hivo Mwanamke alikuwa haoni hasikii mashauri ya wanaomwambiya. Alijitiya kumpenḏa Mwanamume kipofu bila kujali mbeleni iṯakuwa vipi. Katika sehemu ya maelezo ya msimulizi anasema:

104. *Kila ye akiambiwa, wimbo huo siuwimbe*
Yeye hujibu yakuwa, n'taubakiza tembe
Hana la kumtopowa, ela huba za mpambe
Ndwee hii kuuguwa, biniadamu 'siombe.

Juu ya kumfanyiya yoṯ^{h}e hayo Mwanamume alikwenra kupenḏa Mwanamke mwengine aitwaye Mishi. Kwa hivo, kupata alikupenḏeya huku kwa Mwanamke lakini chake na penzi alilipeleka kwa Mishi. Anasema hivi:

15. *Kwa huyo unakopeka, pesa zako mwafulani*
Na leo huko geuka, nenda akakuauni
Apate kukutunuka, akuondowe taabuni
Sikubali kusumbuka, na faida siioni.

Mbali ya Mwanamke kujiṯoleya kwa mali piya alijiṯoleya kwa hali. Anasema kwamba afya yake ilibaḏilika kwa sababu ya kujiṯoleya sana kihali. Anasema:

51. *Deni zikanikondesha, kwa zilivyonizunguka*
Afiya yangu ikesha, na muwili kunyauka
Zikawa zikinikosesha, usingizi ngautaka
Vipi wanambiya kisha, tamaa innishika?

Penzi hili la kuḏanganyana halikuḏumu wakaṯi Mwanamke alipoerevuka na kumjuwa unrani wa Mwanamume: hula kwake lakini akipata chake hukipeleka kwengine. Kwa sababu hiyo Mwanamke naye alimwambiya /nyege ni kunyegezana...huba kwangu zinkwisha/. Fasiri yake ni kwamba kama Mwanamke alivojiṯoleya kumkimu Mwanamume ilikuwa na yeye (Mwanamume) aregeshe fadhila hizo na maaḏamu hakuregesha fadhila basi mapenzi yake hakuna ṯena.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

Abḏilaṯif alijiṯoleya kwa hali na mali mpaka kufikiya haḏi ya kuwa ṯayari kuiṯowa roho yake sabili lakini wanyonge wafaiḏike. Aliṯafuṯa mashini za kuchapisha makala hayo ya kisirisiri, wasambazaji wake mkowani, na kutumiya wakaṯi wake adhimu kwa kuṯayarisha makala hayo. Kwa kuwa mfuwasi shaḏiḏi wa KPU lazima alijiṯoleya haṯa kuhudhuriya mikutano yao ya siri ili kupanga mikakati ya kuenreleza juhuḏi za ukombozi wa wanyonge. Walakini, juu ya yoṯʰe haya wananchi wanyonge hawakusimama naye wakaṯi wa kushikwa kwake, kushiṯakiwa kwake wala kulalamikiya kifungo kikali alichopawa na serikali ya wakaṯi huwo. Aliwachwa pekee kizimbani ajitetee mwenyewe na aliposhinrwa kesini alisukumizwa jela pekee bila ya mtʰu yoyoṯʰe kuṯowa haṯa neno moja. Bali zaiḏi, aliyesababisha yeye kushikwa ni kuhiniwa na rafiki yake mwenḏani wake walokuwa pamoja katika shughuli hii ya kisirisiri. Haya anayasema katika shairi Mja Si Mwema. Na wakaṯi wa kura hizo wananchi walijiṯokeza kuwapigiya washinrani wenzao na kumuwacha yeye pwekee. Hiyana aliyofanyiwa Abḏilaṯif na wananchi inawakilishwa na hiyana aliyofanya Mwanamume juu ya Mwanamke.

Isṯiyara ya wananchi kuḏangana

Baaḏa ya Mwanamume kufukuzwa kwa Mwanamke akaelekeya kwa Mishi ambaye piya alimfukuza akabaki akijizururiya majiyani hajijuwi hajitambuwi. Msimulizi anasema:

153. Furifuri mijitozi, ende huku yamtoka
Ndiya mbili mitilizi, 'kawa yammiminika
Sababu vyake vipenzi, vyote vishamgeuka
Yuwaliya kwa simanzi, aliya asikitika.

154. Akazurura na ndiya, badala kwenda nyumbani
Ovyo akajirangiya, kote mabarabarani
Ni kama alopoteya, au yuko ugenini
Kuliche ilipongiya, bado yu kuzururani.

Mwanamume alikoṯarajiya aṯapata nafuu amefukuzwa na alikoṯumainiya aṯapata afuweni piya hakuipata bali alibakiya katikati hajuwi aenre wapi ṯena. Nrivo ilivoṯokeya kwa mwananchi baaḏa ya mtetezi Abḏilaṯif kufungwa na chama chao kupigwa marufuku. Serikali ya KANU ilichukuwa uwongozi wa kuṯawala Kenya pekee na vyama vengine havikukubaliwa kufanya loloṯʰe. Mwananchi alibakiya kati na kati akiyangaliya mateso juu ya mateso yakiṯiririka moja baaḏa mengine kwa kuṯokuwa na mtetezi wa kuyakemeya maovu yaliyoko. Akabakiya kukubali shingo upanre madhila yoṯʰe anayofanyiwa nriko kuḏangana kwake katika Kutendana.

Kwa hivo, ploti zoṯʰe hizi na jazanra zilizotumika ili kufumba shairi la Kutendana, ni katika ufunḏi wa Abḏilaṯif kuficha masikiṯiko yake juu ya wananchi aliyowapenḏeleya kufaiḏika lakini mwishowe walimhini. Fasiri ya hali halisi ya matukiyo nriyo inayofunuwa siri hii ya Abḏilaṯif kwa kutuonesha namna mambo yalivokwenra. Ni mpaka tuuweke mukṯadha huu wa matukiyo halisi katika fasiri ya shairi hili nripo tuṯakapobaini viwakilishi va wahusika watʰatu na ploti zenyewe zilivosukwa na haswa azimiyo la kujiṯowa siyasani lilikujaje.

AZIMIYO LA ABḎILAṮIF NA NAMNA LILIVOKUJA

Awali tumesema kwamba tukiṯaka kujuwa maana ya kauli ni lazima tuangaliye mukṯadha wa matumizi kama tulivofanya katika sehemu iliyopita. Piya kwamba maneno yamo katika kuathiriyana na kuingiliyana na hivo kuleta maana ṯafauṯi lau neno lile liṯaangaliwa kipekee kama mfano wa kikamusi. Kwa hivo, maana ya neno hupatikana kwa kuangaliwa usuli wake, ujamaa wake na maneno mengine, na historiya ya liṯokako. Kwa minajli hii, katika sehemu hii tuliyangaliya mashairi yoṯʰe katika SyD na namna yalivochangiya kujenga dhamira kuu ya mchezo wa Kutendana. Ni imani yetu, na tuṯathibiṯisha kwa hoja, kuwa shairi hili nrilo la mwisho kuanḏikwa na Abḏilaṯif kifungoni ijapokuwa ḏiwani yenyewe yasema vengine kiṯarehe.

Kwa ujumla ḏiwani ya SyD ina mashairi arobaini yoṯʰe yalianḏikwa kifungoni isipokuwa moja, Nsharudi, lilianḏikwa baaḏa ya kuṯoka. Bila ya kuangaliya ṯarehe zilizowekwa kila baaḏa ya shairi tuṯaona kwamba mashairi haya, kimitinro ya lugha iliyotumika, imegawika katika mafungu matʰatu makuu. Chacha (1992) aliliyelezeya hili la mafungu matʰatu na kuyagawa: fungu linaloonesha Abḏilaṯif si mwoga, ni jasiri wa kunena; fungu la subira na kuwekwa kanro hamasa kali; na fungu la tʰatu la Abḏilaṯif kuruḏiwa na mori wake au hamasa yake ya kuenreleza mapambano. Uchanganuzi wetu umeona vengine kwamba mashairi ya mwanzo

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

yana toni ya hasira alizokuja nazo kuṯoka nje, kwa mfano, Siwaṯi, Nshishiyelo ni Lilo, Mamba. Hasira hizi ameziyeleza katika mahojiyano na Wanjiru (2010). Kisha kuna mashairi ambayo ukiyasoma lugha yake inaonesha Abḏilaṯif ameanza kusoma hali zilivo na kupata welewa wa mambo. Mashairi kama Ah! Mwenzangu, Telezi, Mja si Mwema, Jana na Leo na Kesho yanadhihirisha mtunzi kuanza kufahamu mambo fulani akiwa kifungoni na huwa yana toni ya hali wasṯani siyo ya hasira kama mashairi ya mwanzo. Fungu la t^{h}atu ni mashairi ambayo yanaonesha hali ya utulivu kwa kuweza kuanḏika mashairi ambayo ni marefu yenye uchanganuzi wa fikira zinazoelezwa na hamasa imetoweka kabisa bali ni werevu sasa unadhihiri katika mashairi haya. Mfano wa mashairi haya ni Zindukani, Kichu Hakiwi ni Uchu, Naja, Ndiya Panda na Kutendana. Haṯa Nsharudi japo laonesha hamasa lakini si la kufanya fujo bali kujuwa namna ya kuyapeleka mambo upya kwa njiya baḏali. Ṯafauṯi na Chacha (khj) mwenye kuonesha hamasa katika mwisho wa mashairi ya SyD sisi tumeoneleya mashairi ya mwisho mwisho wa kifungo chake si ya hamasa bali ya kuerevuka na msimamo baḏali na aliyoingiya nawo kifungoni.

Mafungu ya mashairi tuliyoyapiga sisi yameṯokana na kigezo cha ainaṯi za kauli alizotumiya Abḏilaṯif katika mashairi haya. Lakini ifahamike kwamba mpaka alivofikiya kuṯowa azimiyo lake katika Kutendana mambo yalianza kitambo huko nyuma. Kuna kauli mbalimbali ambazo zilipelekeya Abḏilaṯif kuja kusema katika Kutendana /Nyege ni kunyegezana, kwangu huba zinkwisha/. Kama tulivosema hapo awali kuwa tukiiyangaliya ḏiwani hii kama shairi moja kubwa la maisha ya Abḏilaṯif kifungoni bila ya kutizama ṯarehe ama anwani za mashairi tuṯafahamu kuwa mt^{h}u yoyoṯ^{h}e haji kusema neno lenye uzito mkubwa kwa mpigo mmoja bali huwa ni maṯokeo ya kujisaili kwingi na kuṯafakari kuhusu mambo yanavokwenra. Katika jumuiko hilo wakaṯi wa mazishi ya nruguye, Abḏilaṯif alitwambiya kwamba asili ya shairi Kutendana ni beṯi mbili za mwanzo zinazoishiya na maneno hayo tuliyonukuu, halafu akazichangiza mpaka zikafika beṯi 174. Uṯafiṯi wetu ulikuja kugunruwa kuwa maneno haya /...kwangu huba zinkwisha/ yana mfanano na maneno ya babu yake aliyemleya Ahmaḏ Basheikh ambaye alikuwa shekhe na mshairi wa kutajika Ṯ^{h}akaungu na Mambasa. Mfano wa maneno haya yamenukuliwa na Mazrui & Syambo (1992) anapoeleza kuhusu wimbo katika utanzu wa wimbo:

> *Lipi kuu mno, la kunionesha*
> *Ni mengi maneno, na kuhakikisha*
> *Mimi sina neno, **huba zimekwisha***
> (Ahmaḏ Basheikh)

Maneno hayo "huba zimekwisha" ni kwa Kiswahili Sanifu yenye maana sawa na ya Abḏilaṯif "huba zinkwisha" ambacho ni Kimviṯa lugha yake aliyotumiya kwanḏikiya mashairi yake ya SyD. Kwa hivo ni ithibaṯi inayothibiṯisha kauli yetu kwamba neno huṯoka mahali kwengine na kwamba maneno ya sasa ni mwangwi wa maneno yaliyosemwa kitambo cha wakaṯi na mahali. Abḏilaṯif katika ṯamaṯi ya Kutendana aliposema /Kitu n'nachokutaka, shairi wishapo soma. Jaribu kuyaepuka, haya ulosoma nyuma/ swali lililokuja kimbele ni kwa nini msomaji asifanye au asifuwate aliyoyasoma katika shairi hili au ḏiwani nzima?

Uchanganuzi wetu umebaini kuwa mashairi Telezi, Ah! Mwenzangu, Mja si Mwema, Jana na Leo na Kesho, Mambo Yana Mambo Yake, Ndiya Panda, Naja, na Kutendana yana kauli ambazo zinaonesha kuchangiyana kifikra na kumfanya Abḏilaṯif aṯowe azimiyo lake katika Kutendana. Katika Telezi Abḏilaṯif anasema:

6. *Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitiki*
   Bali mimi haamuwa, kwenenda japo kwa dhiki
   Kumbe vile nitakuwa, ni mfano wa samaki
   Ni mfano wa samaki, kuiendeya ndowana.

7. *Zikanibwaga telezi, sikujuwa kuzendeya*
   Ningekwenda kwa henezi, yasingenifika haya
   Lakini tena siwezi, mwendo huwo kutumiya
   Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo.

Mtunzi anaeleza katika shairi hili Telezi kwamba amegeuka samaki katika harakaṯi zake za kupambana na udhalimu wa waṯawala. Hakujuwa anaoingiliyana nao wamemtega kisiyasa. Lau kama alikwenra polepole angejuwa mengi. Katika ṯanabahisho alilopata ni kwamba sasa ashajuwa *namna* (msisitizo wetu) ya kwenra japokuwa haṯokoma huko kwenra.

Katika Ah! Mwenzangu japo shairi lenyewe limelenga kumweleza mt^{h}u mwengine lakini nrani yake anampa funzo ambalo yeye Abḏilaṯif

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

anamṯahadharisha nalo kwa sababu ya ujuzi alonao kuhusu wanasiyasa. Anamwambiya:

7. *Donge la sukari tamu, ambalo melibugiya*
Kati yake muna sumu, kama hujuwi sikiya
Utakuja jilaumu, wakati ukiwadiya
Siseme sikukwambiya, wajipaliya makaa.

Ubeṯi huu unamweleza huyo mwenzake kuhusu siyasa na njama zilizomo nrani yake. Siyasa au vishinro va kisiyasa ni viṯamu lakini vina athari mbaya nrani yake. Anamṯahadharisha huyo rafiki baaḏa ya yeye kujuwa kwamba siyasa ina viṯimvi nrani yake juu ya uḏanganyifu iliyonayo.

Ubeṯi unaofuwata nriyo unaoonesha uzunrushi aliwoupata Abḏilaṯif huko kifungoni kwa kujuwa haswa nani aliyemsaliṯi haṯa akashikwa. Mtunzi anatwambiya tujihadhari naye kwa sababu amemjuwa si mtʰu mzuri. Makosa aloyafanya ni kumwamini (mwananchi) kuwa msiri wake kumbe yule yule aṯakuja kumtiya kwenye nrowana aliyoitaja awali. Katika Mja si Mwema mtunzi anasema:

3. *Mja sikudhani, sikudhaniya, 'tanizunguka*
Nikamuamini, hafikiriya, hatanigeuka
Kumbe mwafulani, hakuzoweya, kuaminika
N'shambaini, ingawa baya, lishanifika.

4. *Menitenda kisa, kisa adhimu, mja mcheni*
Mezinduka sasa, n'shafahamu, najuwa kwani
Ni yangu makosa, najilaumu, kumuamini
Sikuwa napasa, hata sehemu, kumthamini.

Katika Jana na Leo na Kesho ubeṯi wa 11 Abḏilaṯif anasema:

Leo nawe ufunzike, kwa yaliyotuka jana
Makosaye sijitweke, ukayarudiya tena
Sandame hatuwa zake, iwa na hadhari sana
Ya jana ushayaona.

Ubeṯi huu unatueleza kuhusu kusoma na kujuwa mambo yalivo kuṯokana na yaliyotenreka. Anamnasihi Leo (isṯiyari inayowakilisha Abḏilaṯif) kuwa asiruḏiye makosa aliyoyafanya jana awe na hadhari wakaṯi wa kutenra mambo sasa.

Katika shairi Mambo Yana Mambo Yake mtunzi anatweleza namna ya kuingiya katika kufanya kitenro chochoṯʰe haswa ikiwa ni cha kisiyasa chenye kuwakabili waṯawala madhalimu. Mbali ya subira, utulivu, wekevu, na sifa nyengine za kishujaa Abḏilaṯif anaturegesha kwenye kuyaṯaamali mambo siyo kujiingiza kiholela.

13. *Mambo asiyoyajuwa, mtu asiyajaribu*
Kwani yatamsumbuwa, na kumtiya aibu
Sababu hayatakuwa, bure atajipata tabu
Mambo si ya mtu dubu, 'sojuwa kwenda na mambo.

21. *Aliye mtu mwerevu, hali hashindani nayo*
'Kiona hali ni mbovu, haatuwi wake moyo
Huingoja kwa utuvu, hali imruhusuyo
Ijapo akenda nayo, na kuyapeleka mambo.

Mambo hasa ya kisiyasa yaṯaka mtʰu mwerevu na mwenye kujuwa namna ya kupeleka yale mambo. Piya, hakuna kujipasuwa kifuwa ikiwa nafasi baḏo haijakubali. Hivyo, Abḏilaṯif amesoma na kuelewa kwamba nguvu si kila mahali kila wakaṯi bali saa nyengine siyasa huṯaka akili na ṯaraṯibu.

Beṯi zinazokuja tumedonrowa kuṯoka Ndiya Panda kwanza kabla ya Naja kwa sababu uchanganuzi wetu umebaini mḏangano huu ulimpata kabla ya kwamuwa aṯafanya nini kama anavoeleza katika shairi Naja. Katika shairi la Ndiya Panda Abḏilaṯif anaonesha kwamba amefika mahali hajuwi afanye nini maanake amekumbana na njiya mbili zinazomwita koṯʰe kuwili na zoṯʰe zamwonesha kuwa aifwate mojawapo. Abḏilaṯif anasema hivi:

1. *Safari naloiyanza, bado ningalimo kwenda*
Sitawata kujikaza, isipate kunishinda
Nataka kuimaliza, ndivo nipendavyo tenda
Sasa niko ndiya panda.

9. *Ilipofika safari, silijuwi la kutenda*
Nimekwisha kufikiri, lakini limenishinda
Nawatakanyi shauri, nijuwe ndiya ya kwenda
Mojapo ya ndiya panda.

11. *Nnapigwa na pumbao, akili imeniganda*
Kila siku uchao, na mtana nikishinda
Bongo silipi kituo, linijuvye la kutenda
Hukumu ya ndiya panda.

12. *Kila niitupiyao, jito ili kuitunda*
Kila moja kati yao, hunipa ya kunitanda
Huniita: huku ndoo, ni hii ndiya ya kwenda
Yanitanza ndiya panda.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

16. Nichalo ni kujisoza, kisha haja uma vyanda
Ndiponywi hawaambiza, munishauri ya kwenda
Nipani la muwangaza, safari 'sije ivunda
Ajili ya ndiya panda.

Abḏilaṯif ametanzika hajuwi enre wapi au achukuwe njiya ipi iliyo bora kwake. Hivo anaturushiya sisi jukumu la kumwelekeza njiya ipi ya sawa achukuwe. Kwake yeye njiya zoṯʰe ni ngumu: akiwafwata wananchi amewaona unafiki wao na akifwata njiya yake ya kipekee piya baḏo ni dhiki kwa sababu siyasa hawezi kuipeleka pekee. Ilimbiḏi aamuwe njiya aṯakayochukuwa kwa sababu hili aliwachiwa yeye peke yake kifungoni alikuwa hana mshauri na alikataliwa kuzuriwa na mtʰu yoyoṯʰe awe wa karibu (jamaa zake) au wa mbali wanachama wenziye. Walakini, tuelewe kuwa amefika njiya panra na hajuwi achukuwe mwelekeo upi kwa sababu sasa anaogopa kujitumbukiza katika ṯaabu zilizomkumba mwanzo. Woga huu wa kujiyamuliya unamfanya awe ameḏangana. Nripo sana katika shairi Naja tunamwona Abḏilaṯif akijinaki kuwa sasa ameerevuka amesoma kifungoni na ameelewa kila kitu na zaiḏi amefuzu kuyajuwa ya siyasa na njiya zake. Katika shairi Naja anasema:

6. Naja hiwa 'mekomaa, kuzidi nilivo mwando
Tena nnajiandaa, kwa fikira na vitendo
Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

10. Naja na ingawa naja, siwaekei mifundo
Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendewa mwando
Ela wataoningoja, na vyao viwi vitendo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

11. Naja wenye niya hizo, na watotezi vidondo
Naja sitaki matezo, matezo na yawe kando
Naja wakizituwa'zo, 'tawanwisha sichi kondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

Sasa Abḏilaṯif amekomaa kifikra kuliko ilivokuwa mwanzo akiwa hajaingiya kifungoni. Japo amefanyiwa ubaya anasema hana kinyongo wala vita na yoyoṯʰe. Hapo kifungoni amesoma na kupata uzinrushi wa kwamba mambo mabaya aliyofanyiwa: ya kutegewa mtego, kusozwa kwa kuwekwa mbele mbele, kutumiya nguvu kila mahali na wakaṯi, na kuwaamini wananchi sasa amechukuwa njiya nyengine ambayo kimawazo yake iṯawafaa wananchi wake. Katika hali hii ya kwerevuka haingii ṯena vitani kupigana bali mpaka wabaya wake waanze kumṯoṯora nripo aṯakapoingiya kupigana nao anaposema /Naja wakizituwa'zo, 'tawanwisha sichi kondo/ yaani wakiyanza vita yeye aṯaruḏisha vita.

Kauli zoṯʰe hizo tulizonukuu kuṯoka SyD tuṯaona kwamba zinaashiriya kusoma, kupata uzinrushi, kwerevuka na piya kuchukuwa msimamo na mwelekeo mpya kuhusu mambo ya kisiyasa. Tumesema kwamba mpaka Abḏilaṯif alipokuja kufanya azimiyo lake katika Kutendana ilibiḏi apitiye haṯuwa ya kujisaili na kujijaḏili. Kwa hivo, mambo haya ya mivutano ya kifikra hayakuanza siku moja yaweza kuwa ni wakaṯi alipokuwa ashakaa kiḏogo gerezani. Kila hoja aliyoifikiriya ilikuwa ikichangiya na kuathiri uwamuzi aṯakaochukuwa mwisho wa kifungo chake. Nripo sana, Mwanamke alipokuja kumkataa Mwanamume siku hiyo alikuwa ashayaweka kwenye mizani yoṯʰe aliyomfanyiya Mwanamume, hiyana aliyoifanya, na werevu aliwoupata kwa upimaji huwo. Kwanza Mwanamke anamkumbusha Mwanamume kuhusu fadhila alizomfanyiya:

33. Naanza kukukumbusha, kama ushaghafilika
Ni habari 'takupasha, ambazo zintendeka
Nawe 'kiweza jibisha, uonalo lajibika
Au iwa kukanusha, ambalo lakanushika.

34. Nali hijikalifisha, kwamba nipate kuweka
Hifunguwa langu kasha, kila likihitajika
Nikawa nikikulisha, pamoja na kukuvika
Vipi wanambiya kisha, tamaa innishika?

104. Kila ye akiambiwa, wimbo huo siuwimbe
Yeye hujibu ya kuwa, n'taubakiza tembe
Hana la kumtopowa, ela huba za mpambe
Ndwee hii kuuguwa, biniadamu 'siombe.

Mwanamke alipokasirishwa na kwambiwa kwamba ana ṯamaa kuhusu kumpa mwenziwe raha siku hiyo, aliyanza kwa kumkumbusha ya yeye kujiṯoleya kwa hali na mali alimkimu Mwanamume: kumuweka nyumbani, kumlisha na kumvisha. Alipeleleza miyonroko ya Mwanamume kwamba akiwa hana kitu mfukoni yuwajileta kwake lakini akipata chake humpelekeya mwengine. Isiṯoshe, kwa sababu ya mapenzi alonayo kwa Mwanamume Mwanamke

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

akiyambiwa wachana na huyo Mwanamume yeye hukataa. Mwanamke anaenreleya kumfunuliya Mwanamume:

7. Kila mambo naelewa, yaliyo ndiyo na siyo
Si mwana wa kuhadawa, khaswa kwa unambiyayo
Japo wasema ni dawa, sikupi ngakuwa nayo
Na kama yatakuuwa, kufa kwa maradhi hayo.

8. N'lishakupeleleza, hata n'kakubaini
Muda pesa ukijaza, humo mwako mfukoni
Huanza kujikimbiza, na kunigura nyumbani
Ngapita kukuuliza, uliko hujulikani.

Kwa hivo Mwanamke alikuwa ashafanya upelelezi (ashamsoma) miyonroko yake na nriyo baaḏaye akafanya uwamuzi wa kumkataa. Vile vile, kama Abḏilaṯif alivofanyiwa hiyana baaḏa ya kujiṯoleya kwa hali na mali kuhusu siyasa nrivo alivokuja kujuwa baaḏaye kwamba wananchi wamemhini na hapo akaamuwa kuchukuwa haṯuwa ya kufanya azimiyo. Piya Abḏilaṯif alikuja kuonywa na wasimamizi wa mkowa (Chifu Muhammaḏ Fadhiluna wa Mji wa Kale na Mkuu wa Mkowa wa Pwani Isaiah Mathenge katika Wanjiru (2010)) kujiṯowa katika siyasa za hamasa alikuwa haṯaki kwa sababu ya kuwapenḏa wananchi wa chini.

Baaḏa ya kumfunuliya ubaya wake Mwanamke anamwambiya Mwanamume kwamba sasa waepukane na kila mmoja ashike njiya yake. Mwanamke alikuwa ashachukuwa uwamuzi na anasema:

100. Moyoni mwako nitowa, unifute n'siwemo
Mahaba n'shayatuwa, moyoni mwangu hayamo
Siwi wala sitakuwa, kama zamani; horomo! (msisitizo wetu)
Niwapo hivyo 'takuwa, najitiya kwenye shimo.

101.Sasa nihisabu kwamba, n'shakufa kwako wewe
Na kaburi ukatimba, nimo ndani nifukiwe
Siwe na haja kuomba, kurudiyana mi nawe
Kama waweza kuumba, umba mimi mwinginewe.

Beṯi hizi mbili zinaeleza msimamo aliyochukuwa bibi huyu kuhusu Mwanamume. Anamwambiya aonrowe kwenye akili yake kwamba kulikuwa na mtʰu kama yeye na akiweza afukuwe kaburi azikwe humo nrani yake ili amsahau. Kwa sababu ya hiyana zake sasa mahaba yake hayaṯaki ṯena na yashafutika moyoni mwake. Katika kauli tulizozinukuu hapo juu uwamuzi kama huu Abḏilaṯif piya aliuchukuwa baaḏa ya kutambuwa kwamba wale alokuwa akiwaamini kumbe nriyo waṯakaomgeuka.

Azimiyo la Abḏilaṯif kujiṯowa katika siyasa lilikuja baaḏa ya kufanya uwamuzi wa kujiṯenga na wananchi. Katika ubeṯi wa 2 Abḏilaṯif anatwambiya kwamba /Nyege ni kunyegezana/ yaani mtʰu akifanyiwa wema basi hana buḏi kulipa wema ule. Nrivo alivoamini Abḏilaṯif katika maisha yake ya siyasa kwamba wale anawowapiganiya haki zao nao waṯaregesha kwa kumfuwata mawazo yake yenye masilahi mazuri kwao. Lakini hiyana ilipoingiya baina ya Abḏilaṯif na wananchi ikabiḏi aamuwe kubaḏili msimamo wa /kwangu huba zinkwisha/. Kwamba mapenzi baina ya Abḏilaṯif na wananchi katika siyasa ya kijumuiya hakuna ṯena, kila mmoja afwate njiya yake.

Kauli ya mwisho katika Kutendana Abḏilaṯif anasema /Kitʰu n'nachokuṯaka, shairi wishapo soma. Jaribu kuyaepuka, haya ulosoma nyuma/ inazuwa maswali kadhaa: Je, anatwambiya tuonrowe kutenrekezana katika siyasa na kwamba kila mmoja achukuwe jukumu lake kiukamilifu? Au, je, anatwambiya tusiwe kama Mwanamke (Abḏilaṯif) mwenye kujiṯoleya kikamilifu katika siyasa za kijumuiya na filhali hawo anawowapiganiya waṯakwenra kwa wengine pinri wakiḏanganyika? Au, je, anatwambiya kwamba maḏamu penzi la kisiyasa si la kuḏumu kwa kuṯokana na masilahi basi tujuwe kwamba masilahi yakibaḏilika aṯakwenra kwa mwengine ṯu? Rolston (2013) anaeleza kuwa wafungwa huweza kutumiya jela kama mahali pa kujikombowa na kujiweka huru kuṯokana na udhalimu wowoṯʰe, je, Abḏilaṯif akitumiya jela hiyo aliṯaka kujikombowa yeye peke yake na nafsi yake ṯu au na wengine? Je, kauli hii ni nasaha ya Abḏilaṯif kuhusu siyasa ya kujumuiya ambayo Abḏilaṯif anatuṯahadharisha nayo? Ilitubainikiya kwamba Abḏilaṯif alitupa somo kamili kuhusu siyasa ya jumuiya kuṯokana na funzo alilopata yeye, kwa hivo, anawaṯahadharisha wengine au anawakataza wengine wasiingiye mtego wa kupenḏa mapenzi yaliyojengwa na masilahi.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

Mwangwi wa Azimiyo

Maelezo tuloyapata kwa kusoma ṯʰimbo za kisuhufi kumuhusu Abḏilaṯif baaḏa ya kuṯoka kifungoni zimetuthibiṯishiya msingi wetu wa nadhariya kwamba maana ya kauli hupatikana kuṯokana na kuathiriyana kwa maneno katika utungo na kwamba athari hizi zaweza kuwa kwenra mbele au kuruḏi nyuma; kuna mwangwi katika kila neno. Pili, katika upeo wetu wa makala haya tumeeleza kwamba tuṯayachukuliya mashairi ya SyD yanaeleza maisha mamoja mazima akiwa kifungoni. Kwa minṯarafu ya azimiyo na nasaha aliyoiṯowa Abḏilaṯif katika Kutendana juu ya siyasa ya jumuiya, maisha yake baaḏa ya kuṯoka kifungoni yanaonekana kufuwata nasaha hiyo. Kifasihi tuṯasema maisha halisi ya baaḏa ya kifungo ni mwangwi wa mwito wa azimiyo alilochukuwa kinyume na alivosema Chacha (1992) kwamba Abḏilaṯif alionesha kujuṯa kuṯokana na haṯuwa za kisiyasa alizochukuwa, jambo ambalo haṯa Abḏilaṯif mwenyewe anasema katika mahojiyano na Oloo (2003) kwamba hakujuṯa kwani alijuwa anafanya nini na maṯokeo yake yaṯakuwa yapi.

Kulingana na Wanjiru (2010) na Chacha (1992) wanaeleza kuwa Abḏilaṯif alipoṯoka kifungoni alihamiya Tanzania na kushughulika na kazi za kiṯaaluma katika Ṯaasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) sasa Ṯaasisi ya Ṯaaluma za Kiswahili (TATAKI) kama mwanafasihi na mwanaisimu wa lugha ya Kiswahili. Chacha (khj.) anashangazwa na mabaḏiliko haya ya maisha baaḏa ya kifungo lakini hasemi yaṯokana na nini au wapi au kwa nini yaṯokee hivi. Abḏilaṯif alienreleya kutunga mashairi kwa mfano "Nayazinge Mazingawa" (Zinduko, 1974) yenye msimamo kama wa SyD na makala kadhaa kuhusu ushairi. Baaḏaye alihamiya Wingereza kufanya kazi katika shirika la BBC ambako aliweza kuṯayarisha kipinri kimojapo kilichoitwa *Uṯamaḏuni*. Piya alifanya kazi ya uhariri katika gazeṯi la *Africa Events*. Haṯimaye, alijiunga na Chuwo Kikuu cha Leipzig cha Ujarumani kama mwalimu wa Kiswahili haḏi aliposṯaafu 2011. Tuṯaona kwamba waṯafiṯi woṯʰe waliyotutanguliya hawakutaja ni kwa nini Abḏilaṯif alijiṯowa katika shughuli za kisiyasa na kuwa mtʰu wa kanro katika siyasa. Fauka ya hayo, Abḏilaṯif amepawa tʰuzo tʰatu kuadhimisha ushairi wake wa mwamko wa kisiyasa: Jomo Kenyatta Literary Award 1974, Saba Saba Literary Award 1977, na Fonlon-Nichols Award 2018. Tʰuzo ya Jomo Kenyatta Literary Award alikabidhiwa na Rais Jomo Kenyatta mwenyewe katika ikulu ya Nairobi. Je, ni bina kwamba mahasimu wawili wa kisiyasa walikutana na kupaana mikono mwaka mmoja baaḏa ya kuchapishwa mashairi yaliyoṯokana na ṯafauṯi zao za kisiyasa? Jawabu yetu ni yale maneno ya chaguzi za miyaka ya thamanini Mambasa kwamba "siyasa si chuki" likiengezwa na azimiyo alilochukuwa Abḏilaṯif kuwa msimamo wake wa siyasa ya kijumuiya umebaḏilika.

Vinginevo, katika mahojiyano aliyofanyiwa na Oloo (2003), Wanjiru (khj.), na Biermann na wenzake (2011), Abḏilaṯif anasema kwamba walipokuja ṯena yeye na Ngugi na wengine 1982 katika chama cha Umoja wa Kupiganiya Demokrasia Kenya (UKENYA) iliwachukuwa miyaka miṯʰano hivi kujuwana kwa kupaana miṯihani ya uthabiṯi chamani. Miṯihani hii ilikuwa na lengo la kumjuwa nani ana msimamo thabiṯi katika siyasa. Mṯihani wa kumjuwa nani mkweli, nani mrongo, nani msaliṯi kati yao, nani ni barakala, nani mpuuzi amekuja kupoṯezeya wenzake wakaṯi. Swali tunalouliza kwa nini kuṯahiniyana? Je, Abḏilaṯif alicheleya yaliyompata miyaka kumi na tʰatu nyuma yasije yakampata ṯena? Siku zile alijiṯoleya kwa kumwamini mwananchi kwamba wako pamoja, safari hii yaonekana kuṯokana na funzo alilopata kifungoni penzi lake alilipeleka kwa ṯahadhari. Ṯahadhari hizi zinaṯokana na msimamo aliyochukuwa kwamba haṯojiingiza ṯena katika siyasa za kijumuiya kwa sababu ya haḏaa zilizomo nrani yake. Juu ya hayo, kujiṯowa huku kuliṯokana na azimiyo alilofanya wakaṯi akiwa kifungoni kwamba hamwamini ṯena mwananchi.

Kujiṯowa huku kunatiliwa nguvu na ṯashwishi aliyonayo kuhusu haṯa siyasa ilivogeuka nchini Kenya. Katika wasilisho linalorejeleya makala yake ya *Kenya Twendapi?* alilofanya 2015 hapo Kenya Cultural Centre, Nairobi, baḏo yeye anaona shere ṯu katika siyasa ya Kenya Mpya (baaḏa ya 2002). Kwa sababu komba ni wale wale msitu ṯu umebaḏilika – wanaKANU baḏo wamo katika serikali, wakaṯi huwo, ya Mwai Kibaki (kwenye mahojiyano na *Radio Salaam*, Mambasa, 2012). Anasema baḏo wananchi wanateseka na waliyo mamlakani wanaenreleya na njama zao kujinufaisha wao na kuwakanramiza wananchi masikini. Walakini Abḏilaṯif, tujuwavo sisi, si

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

mwanachama wa chama chochoṯʰe cha kisiyasa nchini Kenya isipokuwa amekuwa akiṯowa maoni yake ya kisayasa katika kumbi mbalimbali ulimwenguni. Hali hii ya ukimya sasa nriyo inayotupa sisi mshawasha wa kusema kwamba azimiyo lake alilofanya kifungoni baaḏa ya funzo alilopata limemfanya awe mkimya wa kuyaṯathmini mambo lakini siyo kujitiya mzima mzima.

HIṮIMISHO

Makala haya yalikuwa na lengo la kuonesha kuwa Abḏilaṯif Abḏalla alivoingiya kifungoni 1969 alikuwa ni mtʰu mwenye hasira nyingi kuhusu siyasa inayoenreleya katika jamii yake ṯafauṯi na alipoṯoka miyaka mitʰatu baaḏaye. Alipoṯoka, Abḏilaṯif alikuwa mtʰu mkomavu, mtulivu, mkimya, na zaiḏi hamasa za siyasa ya kijumuiya zimemwishiya kutokana na funzo alilopata baaḏa ya kujisaili na kujaḏiliyana na nafsi yake huko gerezani.

Tumejaribu katika makala haya kulishughulikya shairi Kutendana katika ḏiwani ya SyD kwa namna ṯafauṯi na waṯafiṯi waliyotutanguliya waliyoliyangaliya shairi hili kama la unyumba. Sisi tumejaribu, kwa kutumiya nadhariya ya Usemezano na Uhistoriya Mpya, kuṯowa ufumbuzi mwengine wa shairi hili kwa kuangaliya namna maana ya neno linavojulikana kwa mwingiliyano wa neno hilo na mukṯadha, historiya, usuli, ujamaa wake na maneno mengine na niya ya msemaji wa neno hilo. Piya tumeliangaliya neno hilo likiwa na athari liṯokako na linavoathiri maneno yanayokuja baaḏa yake.

Makala haya yameweza kuchanganuwa baadhi ya isṯiyara na kauli zilizotumika ili kubayanisha kwamba shairi hili nriyo fumbo la Abḏilaṯif kujihusisha na siyasa za kijumuiya. Isṯiyara ya wahusika watʰatu: Mwanamke, Mwanamume, na Mishi (mwanamke mwengine) nriyo kiwakilishi cha mapote ya kisiyasa yaliyokuwako nchini Kenya baaḏa ya uhuru, yaani, KANU na KADU, KPU na wananchi wa ṯabaka la chini. Isṯiyara hii inaonesha namna Abḏilaṯif ambaye anawakilishwa na Mwanamke anajiṯoleya katika kuenreleza harakaṯi za kuwatumikiya wananchi wanaowakilishwa na Mwanamume. Mapenzi yao ni ya kihawara wala si ya nrowa kishariya kwa hivo masilahi yalipokatika baina ya wahusika hawa wawili, Mwanamke aliyona hakuna haja kukaa na mtʰu mwenye hiyana. Kiufafanuzi wetu Abḏilaṯif alijiṯoleya kwa hali na mali haṯa kuhaṯarisha maisha yake ili wananchi wafaiḏike lakini ilipofika wakaṯi wa kumteteya yeye au kukipa kura chama chake KPU walimhini na kukipa chama cha KANU ambacho baaḏa ya muḏa kiliṯupa mipango ya kuwanufaisha wao na kushika njiya ya kuwanufaisha wanasiyasa walafi wachache.

Abḏilaṯif alipoyaona haya ya hiyana na kusaliṯiwa na msiri wake haḏi kusababisha kufungwa, huko kifungoni alikuwa mkali mwanzo lakini baaḏa ya kusoma hali ilivo alikuja kupata uzinrushi uliyomfunuwa mawazo yake. Kuṯokana na mwingiliyano wa kauli mbalimbali tulizochota kuṯoka mashairi ya mwanzo wa aingiyapo haḏi afikapo Kutendana tulipata kuwona kuwa Abḏilaṯif alifunzika na baaḏaye kufanya azimiyo ambalo nrilo linalobaḏilisha maisha yake ya baaḏa ya kifungo. Zaiḏi ya hayo, anawanasihi na watʰu wengine wajaribu kwepuka kufuwata siyasa ambazo hazina mashiko thabiṯi. Kwetu sisi, Abḏilaṯif alipata funzo na akafanya azimiyo huko huko kifungoni na hapo kuthubuṯu kauli ya babu yake aliyomwambiya alipoṯoka kifungoni kuwa siyasa ni tʰanga si nanga yaani ikiwa siyasa haina makhlasa na fikra zako basi geuza misimamo yako kama tʰanga kufuwata upepo upigako wala siyo kukʰita kama nanga. Kuṯokana na funzo alilopata kifungoni yaonekana Abḏilaṯif alifuwata msimamo wa kujiṯowa siyasa za kijumuiya na kushika msimamo wa nafsi yake peke yake.

Uchanganuzi wetu kuṯokana na shairi hili na yoṯʰe mengine yaonesha baḏo pana mengi yanaweza kuṯafiṯiwa: kwa mfano, aina ya lugha ya *skaz* (lugha ya watʰu wa kawaiḏa) aliyotumiya Abḏilaṯif inaweza kutupa ufafanuzi upi zaiḏi? Piya, kuṯokana na shairi hili tunaweza kuṯafiṯi je, sauṯi ya dhiki ya Abḏilaṯif inaṯokana na dhiki ya kifungo au msimamo mpya aliyoutwaa wa kujiṯenga na siyasa za kijumuiya? Tʰatu, pana haja kubwa ya kujuwa ṯawasifu na mikṯadha ya kuanḏikwa shairi hili, bali mashairi yoṯʰe ya SyD, ili tujuwe mengi kuhusu maisha yake kifungoni. Ni neema kubwa kwamba baḏo yuko, Mungu Amuweke, na anaweza kutueleza mengi, kwa mfano, shairi Muosheni ni nani?, shairi Leo Nsingekuwako kuliṯokeya nini? Shairi Wasiwasi Enra Zako aliyambiwa nini? Yo

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

t̠^{h}e haya ni katika kut̠owa ufumbuzi wa hizo fasiri 1001 alizoahid̠i Abd̠ilat̠if kuwapa maaskari wa gereza lau angeshikwa na mashairi haya ya SyD.

MAREJELEO

Abdalla, A. (2012). *Sauti ya dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.

Abdalla, A. (1985, September). The right and might of a pen. *Africa Events*, Once upon a time, uk. 25-26.

Abdalla, A. (2015, Disemba 7) Kenya Twendapi? Na Abdilatif Abdalla [video file]. Imesomwa: https://www.youtube.com/watch?v=0soJOZjjCc4

Bakhtin, M. M. (1981). *Dialogic Imagination: Four essays*. M. Holquist (mh.), C. Emerson & M. Holquist (wat̠afsiri). Austin: University of Texas Press.

Beck, R. M. & Kresse, K. (wah). (2016). *Abilaif Aballa: Poet in politics*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Biermann, S., Richards, N. & Milbourne, M. (2011, Mei). We Harvest the Present from the Future We Planted Yesterday. Mahojiyano na Abdilatif Abdalla and Ngugi wa Thiong'o, Leipzig, Ujarumani.

Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya utetezi*. Dar Es Salaam: Dar Es Salaam University Press.

Gibbe, A. G. (1978). Fasihi na jamii baadhi ya washairi wa Kiswahili 1960-1977. Katika *Kiswahili 48* (1), 1-25.

Habib, M. A. R. (2005). *A history of literary criticism*. Malden: blackwell Publishing.

Hamad, M. A. (2017). *Suala la ufungwa katika ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka diwani za Sauti ya dhiki na Chembe cha moyo*. T̠asnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuwo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Karanja, M. W. (2014). *Matumizi ya istiari, tashbiha na taashira katika diwani ya sauti ya dhiki*. T̠asnifu ya Uzamili (Haijachpishwa), Chuwo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Khamis, S. A. (2016). Whither Swahili literature? Translation and the world recognition of Abdilatif's "sauti ya dhiki". Katika R. M. Beck & K. Kresse (wah). *Abdilatif Abdalla: Poet in politics*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota. UK. 35-44.

Kindy, H. (1971). *Life and politics in Mombasa*. Nairobi: East African Publishing House.

Maitaria, J. N. & Wafula, R. M. (2018). Ushairi wa Abdilatif Abdalla katika kubainisha utamaduni wa Waswahili. Katika *Journal of Linguistics and Language in Education 12* (2), 74-92.

Mazrui. A. & Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mazrui, A. (2017, Novemba). Abdilatif and I: Reflections on comparative experiences. Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la "The imaginative vision of Abdilatif Abdalla: Kenyan poet and activist" Princeton University, Princeton.

Mulokozi, M. M. (1975). Revolution and reaction in Swahili poetry. Katika *Kiswahili 45* (2), 46-65.

Mwamzandi, I. Y. (1996). *Mbinu za kimaigizo katika ungo za Abdilatif Abdalla*. T̠asnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuwo Kikuu cha Egerton, Njoro.

Odinga, O. (1968). *Not yet uhuru: An autobiography*. Nairobi: Heinemann.

Ohly, R. (1974). A review of Abdilatif Abdalla's *Sauti ya dhiki*. Katika *Kiswahili 44* (2), 82-91.

Oloo, O. (2003, Februari). Mahojiyano na Abdilatif Abdalla. Imesikizwa: https://web.archive.org/web/20030630105524/http://vancouver.indymedia.org/news/2003/02/32103.php 01/10/2019.

Said, Z. & Taib, A. H. (2019). *Fasihi ya ufungwa: Nadharia na mikabala ya uhakiki – riwaya kama kifani*. Dar es salaam: Heko Publishers.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.144

Salim, A. I. (1975). *Swahili speaking peoples of east africa 1895-1975*. Nairobi: East African Publishing House.

Senkoro, F. (1988). *Ushairi: Nadharia na tahakiki*. Dar Es Salaam: Dar Es Salaam University Press.

Shafi, A. (2003). *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers

Shariff, I. N. (1988). *Tungo zetu: Msingi wa mashairi na tungo nyinginezo*. New Jersey: The Red Sea Press.

Topan, F. (1994). Chacha Nyaigotti Chacha, *Sauti ya utetezi: Ushairi wa Abdilatif Abdalla*: *A review*. AAP 37, 197-198.

Topan, F. (2006). Why does a Swahili writer write? Euphoria, pain, and popular aspirations in Swahili literature. Katika *Research in African Literatures 37* (3), 103-119. Imesomwa: https://www.jstor.org/stable/3821182. 18/10/2019.

Tyson, L. (2006). *Critical theory today: A user-friendly guide* (Toleo la 2). New York: Routledge.

Walibora, K. (2009). Prison, poetry, and polyphony in Abdilatif Abdalla's *Sauti ya dhiki*. Katika *Research in African Literatures 40* (3), 129-148.

Walibora, K. (2016). Doing things with words in prison poetry. Katika R. M. Beck & K. Kresse (wah). *Abdilatif Abdalla: Poet in politics*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota. UK. 55-64.

Wanjiru, K. (2010). Abdilatif Abdalla: My poems gave me company. Imesomwa: https://www.pambazuka.org/arts/Abdilatif-Aballa-my-poems-gave-me-company tarehe 22/10/2019.

Vierke, C. (2017). What is there in my speaking: Re-explorations of language in Abdilatif Abdalla's anthology of prison poetry, *Sauti ya dhiki*. *Research in African Literatures 48* (1) 135-157 Doi: 10.2979/reseafrilite.48.1.09.